

# JARIDA LA UWEZESHAJI



Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)

Agosti 2017

## TOLEO LA NNE



[www.uwezeshaji.go.tz](http://www.uwezeshaji.go.tz)

## YALIYOMO

|  |    |
|--|----|
| 1. Neno kutoka kwa Katibu Mtendaji.....                                    | 3  |
| 2. NEEC yatambua makundi ya Uwezeshaji.....                                | 5  |
| 3. Vijana watakiwa kujenga nidhamu ya fedha.....                           | 10 |
| 4. NEEC yasaini mkataba wa ushirikiano na TSN.....                         | 11 |
| 5. Waziri Mkuu azindua maonyesho ya mifuko ya Uwezeshaji ya Seri-kali..... | 12 |
| 6. Waziri Mkuu anunua hisa za Vodacom.....                                 | 14 |
| 7. Baraza laratibu mkakati wa kitaifa wa uendelezaji Wajasiliamali.....    | 16 |
| 8. NEEC ni kiongozi katika safari ya kuwezesha Wananchi Kiuchumi.....      | 18 |
| 9. NEEC yaanika fursa za Uwezeshaji katika mradi wa bomba la mafuta...23   |    |
| 10.Habari katika picha.....  | 25 |

# Neno kutoka kwa Katibu Mtendaji

Ndugu msomaji, karibu katika toleo la nne la jarida hili linalohusu Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), majukumu na mafanikio yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Toleo hili linaleza kwa mapana juu ya majukumu yaliyotekeliza na Baraza katika mwaka wa fedha 2016/2017 katika kuhakikisha Watanzania wanawezeshwa Kiuchumi kama ilivyoainishwa katika Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 .



Baraza limekamilisha uteuzi na utoaji wa mafunzo ya uwezeshaji kwa waratibu wote kuanzia ngazi ya Mikoa na Wizara.

Tunafurahi kufanikisha uanzishwaji wa madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Wizara zote 20, Idara, Taasisi 58, Mikoa 26 na Halmashauri za Miji na Majiji 185.

Mafunzo ya utekelezaji wa majukumu katika madawati haya yametolewa nchi nzima ambapo yalishirikisha Wakuu wote wa Mikoa, Makatibu Tawala,Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Miji,Maafisa Mipango na Waratibu wa Uwezeshaji ngazi ya Mikoa na Halmashauri nchini. Ripoti ya pili ya uratibu wa uwezeshaji kiuchumi ilizinduliwa rasmi mwezi Julai 2017 ambapo imeanisha kwa kina utekelezaji wa uratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi hapa nchini.

Baraza limefanikiwa kuratibu suala la ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji hapa nchini kwa kuainisha maeneo matano ya kipaumbele ili kumrahisishia Mtanzania kuona fursa mpya za kiuchumi.

*inaendelea uk.4*

Maeneo hayo ni kuunda mfumo wa uratibu wa masuala ya ushiriki wa Watazania katika uwekezaji, kuendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu uwekezaji, kufanya tafiti bainifu kuhusiana na uwekezaji katika sekta za madini, gesi, kilimo na ujenzi, kufanya mikutano na wadau wa sekta za kilimo, ujenzi na madini ili kubaini changamoto za Watanzania kuweza kushiriki katika uwekezaji unaofanyika hapa nchini .

Ili kupanua Elimu na wigo wa masuala ya uwezesaji wananchi kiuchumi, Baraza linafanya kazi zake kwa uwazi baada ya kuingia makubaliano na Kampuni ya Uchapishaji Magazeti ya Serikali, TSN kitakuwa chombo rasmi katika kutoa taarifa mbalimbali za Baraza kwa maslahi ya umma.

Baraza pia limeendelea kutoa dhamana ya mikopo kwa vikundi vyta uzalishaji mali, SACCOSS na VICOBA hapa nchini kupitia amana yake iliyopo kwenye taasisi ya fedha ya TPB PLC.

Mpaka kufika mwezi Juni mwaka huu Baraza limeweza kutoa ufadhili wa mikopo yenye thamani ya shilingi Bilioni 1.488 kwa wanaume 372 na wanawake 1044 katika mikoa ya Pwani, Kagera, Dar es Salaam, Tabora, Ruvuma, Iringa, Tanga na Kigoma.

Baraza pia limetanua huduma hiyo kwa kuingia makubaliano na Taasisi ya fedha ya UTT Micro-finance PLC ambao wataanza kutoa mikopo kwa makundi ya uzalishaji mali ya vijana ambayo yanajiendesha kwa mfumo wa SACCOSS na VICOBA.

Baraza pia lilifanya Kongamano la Pili la uwezesaji Mjini Dodoma na kukutanisha wadau mbalimbali toka sekta za Umma n Binafsi na wadau wa maendeleo.

Katika kuchochea utekelezaji wa Sera ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na kufikia dira ya Baraza, mgeni rasmi wa kongamano hilo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Bunge Mheshimiwa Jenista Mhagama alitoa tuzo za vikombe na vyeti kwa washindi toka ngazi za Mikoa, Wizara, Idara na Sekta binafsi ikiwa kama njia ya kutambua michango mbalimbali iliyotolewa.

Kongamano hili linatarajiwa kufanyika kila mwaka kwa lengo la kukutanisha wadau wa sekta ya umma na binafsi na kushirikishana namna bora zaidi ya kuchochea uwezesaji wananchi kiuchumi hapa nchini.

### **Bi Bengi Issa Katibu Mtendaji**

## NEEC yatambua makundi mbalimbali yanayowezesha jamii kiuchumi



*Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu, sera Na Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama akimkabidhi kikombe Kaimu Mkurugenzi wa wateja wakubwa wa Benki ya NMB, Michael Mungure wakati wa Kongamano la pili la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi lililofanyika Mjini Dodoma*

KATIKA kuchochea utekelezaji wa Sera ya Uwezesaji Wananchi kiuchumi ya mwaka 2004, Baraza limetoa tuzo mbalimbali kwa washindi kuanzia ngazi za Mikoa, Wizara, Idara, Taasisi za Umma, Sekta Binafsi na mifuko ya uwezesaji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jennista Mhagama alikabidhi tuzo hizo kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa katika

Kongamano la pili la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi lililofanyika katika Ukumbi wa Wizara ya Fedha mjini Dodoma, lengo likiwa ni kuwawezesha Watanzania kushiriki Uchumi wa Viwanda ambayo ndio dira ya Serikali ya awamu ya tano.

Kongamano lilihudhuriwa na wajumbe wasiopungua 300 kutoka idara za Serikali, Wizara, vyo, ofisi za kibalozi, sekta binafsi. S Viongozi wa kitaifa wakiwemo Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wa Taasisi za Umma na binafsi hapa nchini nao walihudhuria.

Katibu Mtendaji wa Baraza, bi Beng'i Issa alieleza malengo ya kongamano hilo kuwa ni kuwawezesha Watanzania kushiriki Uchumi wa Viwanda, kupeana uzoefu katika masuala ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi, kutambua michango mbalimbali ya uwezeshaji kutoka Sekta za Umma na Binafsi pamoja na kuibua fursa mpya za Uwezeshaji Wananchi kiuchumi ili kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa.

Hotuba ya Katibu Mtendaji pia ilitambua michango ya wafadhili waliowezesha uwepo wa Kongamano wakiwemo Maxcom Africa, TSN, NMB, VODACOM, UNDP, Clouds FM, Cocacola kwanza, TPB Bank, Kamal Steel LTD, African Risk and insurance services ltd, MIVARF Project, GE Oil and Gas, EU, NSSF, UTT Microfinance, ASAS Group, African Media, NRGI na UTT AMIS ambao kwa pamoja walipewa vyeti na mgeni rasmi.

Katika ngazi ya Mikoa, nafasi ya kwanza ilikwenda Mkoa wa Simiyu huku nafasi ya pili ikienda Mkoa wa Morogoro na nafasi ya tatu ilichukuliwa na Mkoa wa Kigoma

Kundi la pili lilihusisha Wizara, Idara na Taasisi za Umma na wakala ambapo nafasi ya kwanza ilichukuliwa na Wizara ya Kilimo, ufügaji na Uvubi huku nafasi ya pili ikinyakuliwa na Shirika la viwango (TBS) na nafasi ya tatu ikichukuliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa manunuzi ya Umma (PPRA) ambao pia walipewa tuzo ya vikombe.





Katika kundi la Sekta binafsi,nafasi ya kwanza ilichukuliwa na Benki ya NMB ikifuatiwa na Vodacom Tanzania na Clouds Media.

Kwa upande wa mifuko ya Uwezesaji nafasi ya kwanza ilichukuliwa na TA-SAF, ya pili ilienda kwa SELF Microfinance wakati mfuko wa uendelezaji wajasiliamali (NEDF) wakikamata nafasi ya tatu na kukabidhiwa vikombe.

Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini.




(MIVARF) ilipewa tuzo maalumu kwa kutekeleza vyema sera ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi katika mradi wake.

Ili kufanikisha hazma yake ya Kuwezesha Wananchi Kiuchumi, Kongamano hilo liliandaa majadiliano ya kubadilishana uzoefu

kutoka kwa Wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi ili kushawishi mabadiliko ya kisera na sheria yatakayopelekea kasi ya kuchochea uwezesaji wananchi kiuchumi. Miiongoni mwa wadau walioshirikisha uzoefu wao ni pamoja na

Mkurugenzi wa Alaska, Jennifer Bash, Juma Rajab kutoka Maxcom Africa, Godius Kyarahara wa NSSF, John Kyaruzi wa SAGCOT, Audax Lukonge wa TANSAF, DR Jimmy Yonanzi kutoka TSN, DR Astronat Bagile wa WISE/NEEC, Gilead Terry kutoka TPSF, Revocatus Kimario wa SUGECO na RC John Mtaka.

Wajumbe waliuliza maswali kwa watoa mada ili kujifunza njia mbalimbali za kuelekea kwenye mafanikio ya kiuchumi.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi, NEEC Bi Beng'i Issa akibadilishana hati ya makubaliano ya dhamana ya mikopo na Mkurugenzi wa Taasisi ya miradi midogo ya fedha, UTT Microfinance PLC

## Vijana watakiwa kujenga nidhamu ya fedha za mikopo

VIJANA walionufaika na mafunzo ya ujasiliamali chini ya Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) wametakiwa kuheshimu fedha za mikopo walizopewa na kurejesha kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kupata.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo,Bi Beng'i Issa alisema hayo wakati wa utilianaji saini ya makubaliano ya udhamini wa mikopo toka kwenye taasisi ya fedha,UTT Micro Finance PLC jijini Dar es salaam.

Tunalo tatizo kubwa la ajira hapa nchini na njia pekee ni kuwafundisha vijana elimu ya ujasiliamali na kuwapatia mikopo ili waweze kuendeleza miradi itakayowakwamua kiuchumi"alisema Katibu Mtendaji.

"Baraza linafanya kazi kubwa ya kuwezesha vijana kupata mitaji.Baraza limesaini makubaliano ya udhamini wa mikopo inayotolewa na taasisi ya fedha, Micro finance".

Bi Being'i Issa aliongeza kuwa zimetengwa shilingi milioni 300 ili kudhamini mikopo ya shilingi bilioni moja ambayo itatolewa katika miradi mbalimbali ya vijana.

Miradi inayopewa kipaumbele katika ufadhili huo ni pamoja na usindikaji,uongezaji wa thamani ya mazao,ufugaji, vifaa vya kilimo,uvuvi na usafirishaji.

Mpango huo pia unaangazia miradi inayotumia malighafi za ndani na yenye uwezo wa kutengeneza ajira hasa kwa vijana wa Taifa hili.

Ili kuweza kunufaika na udhamini wa mikopo hiyo yenye masharti na-fuu, vijana wanatakiwa kuwa na SACCOS zenye sifa kwa mujibu wa sheria ya vyama vya Ushirika na vi-kundi vya uzalishaji mali.

# NEEC yasaini mkataba wa ushirikiano na TSN

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, (NEEC) lasaini hati ya makubaliano na Kampuni ya uchapishaji magazeti ya Serikali, TSN ili kuhabarisha Wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi.

Mkataba wa Baraza na TSN unalenga kuhamasiha na kuelimisha jamii kuhusiana na masuala ya kiuchumi kuititia magazeti ya Daily News, Habari Leo,spoti leo na Sunday news ambayo yanazalishwa na kampuni hiyo kongwe hapa nchini.”

Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi Beng'i Issa amesema kuwa wameingia makubaliano na TSN kwasababu wanaamini katika uzoefu na upana wa kampuni hiyo katika tasnia ya habari hapa nchini kuweza kuwafikia Watanzania wengi katika kila pembe ya Taifa hili.

TSN kama chombo cha Serikali kitawajibika moja kwa moja katika kuhabarisha Umma juu ya umuhimu wa kutekeleza Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na utekelezaji wake.

“Tumesaini makubaliano haya na TSN ili kuona namna ya kuwafikia Watanzania wote kuweza kuwapasha masuala mbalimbali yanayohusu elimu uwezeshaji kiuchumi kwa Taifa hili”alisema Katibu Mtendaji.

Baraza kazi yetu ni kuratibu, kuunganisha na kufuatilia lakini suala la utekelezaji wa sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumu ni la kila Taasisi,Wizara na Idara zote za Umma na binafsi hivyo TSN kama chombo cha Serikali kitawajibika moja kwa moja katika kuripoti masuala yote haya”.

“Tumewapa wao dhamana ya kupeleka ujumbe kwa Taifa zima kwasababu ya upana wao na uwezo wa kufika kila pembe ya nchi hii kuititia magazeti yao”.

Nae Mhariri Mtendaji wa kampuni ya TSN, DKT Jim Yonazi alisema kuwa kampuni ya TSN itafanyakazi bega kwa bega na Baraza ili kuelimisha wananchi kushiriki uchumi unaokusudiwa na Serikali ya awamu ya tano ambayo imelenga katika kuchochea maendeleo ya viwanda hapa nchini.



*Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bi Beng'i Issa akisaini hati ya makubaliano na Mhariri Mtendaji wa Kampuni ya magazeti ya Serikali TSN, DR Jimmy Yonazi juu ya uchapishaji wa taarifa za uchumi na elimu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.*

*inaendelea uk.12*

## Waziri Mkuu azindua maonyesho ya Mifuko ya Uwezesaji Dodoma



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa akizungumza na wajasiliamali wakati wa maonyesho ya Mifuko ya Uwezesaji Mjini Dodoma. Kulia kwake ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama.*

Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), limezindua maonyesho ya mifuko ya Uwezesaji Mkoani Dodoma ukiwa ni mkakati wa utekelezaji wa sera ya Taifa ya Uwezesaji ya mwaka 2004.

Maonyesho hayo yalizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa katika viwanja vya mashujaa lengo likiwa ni Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi, kujenga Uchumi wa kati na Tanzania ya Viwanda.

Mifuko inayoshiriki katika maonyesho hayo ni Mfuko wa kuendeleza wajasiliamali Wananchi, Mfuko wa Uwezesaji wa Mwananchi, Mfuko wa pembejeo za Kilimo, Mfuko wa Men-deleo ya Vijana, Mfuko wa dhamana ya mikopo kwa wajasiliamali wadogo, wa kati na mfuko wa mikopo kwa mauzo ya nje ya Nchi.

Mifuko mingine ni Mfuko wa kuwasaidia Wakandarasi, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii na Mfuko wa misitu Tanzania.

Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi Beng Issa amesema kuwa lengo la maonyesho ya mifuko ni kutoa elimu kwa Umma juu ya huduma mbalimbali zitolewazo na mifuko yote ya Uwezeshaji hapa Nchini.

"Maonyesho yalikuwa na lengo la kuwapa watu fursa ya kuonana na watu ambao wamefanikiwa katika kipindi kilichopita na hasa kujua jinsi gani watafaidika na mikopo ambayo inapatikana kupitia mifuko hii" alisema Katibu Mtendaji.

"Tuliamua kufanya maonyesho kwa mara ya kwanza kwasababu changamoto kubwa tuliyonayo ni kuwa Wananchi wengi walikuwa hawajui wafanye nini ili waweze kupata fursa za mitaji na kusaidiwa na mifuko ambayo imeanzishwa na Serikali kwa ajili yao" aliongeza Bi Beng'i.

Maonyesho ya Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni ya kwanza kufanywa na Baraza ambapo limedhamiria kuhakikisha inafahamika na kunufaisha kila mhitaji na hasa Wajasiliamali na vikundi vyta uzalishaji Mali.



# Waziri Mkuu anunua Hisa za Vodacom

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa amenunua hisa zenyet thamani ya shilingi Milioni 20 toka kwenye kampuni ya simu za mkononi, Vodacom ambayo imemua kutoa sehemu ya umiliki wake kwa Wananchi.

Waziri Mkuu alichukua hatua hiyo mbele ya Viongozi wa Baraza la Uwezesaji Wananchi Kuuchumi (NEEC), wakuu wa masoko ya hisa na dhamana na wafanyakazi wa idara ya masoko Vodacom. Zoezi la ununuzi wa hisa hizo lilifanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Waziri Mkuu iliyopo Magogoni jijini Dar es salaam.

Wadau wengine walioshudia tukio hilo ni pamoja na Waziri wa fedha na Mipango Mheshimiwa Philip Mpango, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana Nassma Masinda.

Wakati wa ununuzi wa hisa hizo, Waziri Mkuu alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ya Kiuchumi kwa kununua hisa za Vodacom haraka kabla muda haujaisha.

kwa kununua hisa za Vodacom haraka kabla muda haujaisha "Hii ni fursa kwa Watanzania kuwa sehemu ya umiliki wa




kampuni ya Vodacom, ukinunua hisa hapa maana yake na wewe ni mmiliki wa kampuni" alisema Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa.

"Ni jambo zuri kwa Wananchi kuwekeza wakati huu na hasa fursa zinapojitokeza kama hii ya Vodacom nawataka wananchi wa-changamkie jambo hili".

Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Hisa, Nassama Masinda alisema kuwa amefurahishwa kuona Waziri Mkuu akijitokeza hadharani kununua hisa hizo na kutoa motisha kwa Wananchi kuchangamkia fursa hii.

*inaendelea uk.15*

Huku Mtendaji Mkuu wa Vodacom, Ian Farrao akieleza kuwa kampuni yake imewekeza zaidi ya Trilioni mbili kwenye huduma ya mawasiliano hapa nchini lakini pia uuzwaji wa Hisa unaofanyika hivi sasa ni mara nne ya ukubwa wa mauzo ya hisa ambao umewahi kufanywa miaka ya nyuma.



## Baraza laratibu uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Uendelezaji Ujasiriamali Nchini.

Watanzania wametakiwa kutumia fursa zinazoendelea kuwekwa na serikali ya awamu ya tano kujikita katika ujasiriamali na kuanzisha viwanda kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda ili kufikia uchumi kati na kuboresha ustawi wa jamii hapa nchini Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Profesa Adolf Mkenda alisema hayo wakati wa mukutano wa wadau kutoka sekta ya umma na binafsi uliokuwa ukijadili rasimu ya mapendekezo ya mkakati wa kitaifa kuendeleza ujasiriamali hapa nchini.



"Wakati wa watanzania kuanzisha viwanda kuzalisha bidhaa zinazotokana na mali ghafi za hapa nchini umewadia," na hakuna wakati mzuri zaidi kuliko kipindi hiki ambacho serikali imewe ka kipaumbele zaidi katika hili, aliongeza kusema Profesa Mkenda.

Mkakati huo wa kitaifa wa kuendeleza ujasiriamali umeandaliwa na Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa ushirikiano wa utaalamu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa Linalojihusisha na Maendeleo ya Biashara (UNCTAD).

Profesa Mkenda alifanua kwamba serikali imeamua kuja na rasimu hiyo kupata maoni ya wadau ili kukamilisha Mkakati wa Taifa wa Uendelezaji Ujasiriamali nchini.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bi. Beng'i Issa alisema Baraza lake linasimamia sera ya uwezesaji wananchi kiuchumi na suala la ujasiriamali ni nguzo muhimu katika uwezesaji wananchi kiuchumi.

"Pendekezo la mkakati huu wa kuendeleza ujasirimali umeandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na leo ni siku ya pekee kwa wataalaam kutoa maoni yenu ili kupata mkakati wa kitaifa," na aliwaomba wataalamu hao kutoa maoni yao kwa uwazi ili kukamilisha upatakanaji wake, alisema, Katbu Mtendaji.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Prof Adolph Mkenda akifungua mukutano wa kuandaa mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza ujasiriamali nchini.

Alisema jukumu la kuandaa mkakati wa kitaifa wa kuongoza ujasiriamali kufikia uchumi wa kati na wa viwanda ni muhimu kwa vile utawezesha kupata wajasiriamali wenye mafanikio waliongozwa vyema.

Alisema uandaaji wa rasimu hiyo umeangalia mapungufu yaliyopo katika uendelezaji wajasiriamali hapa nchini na umekuja na majibu ambayo ni rafiki kwa wajasiriamali.

Alisema hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Agosti 2017 maoni yote ya wadau yatakuwa yameingizwa na matarajio yaliyopo ni kwamba mkakati huo utaweza kuwa tayari mwezi Octoba 2017

kwa ajili ya uzinduzi rasmi tayari kwa kutumia na wadau mbali mbali kama walivyoanishwa katika mpango kazi wake kwa utekelezaji kwa lengo kuendeleza ujasiriamali nchini kwa kasi zaidi.

Mkakati wa Taifa wa Uendelezaji Ujasiriamali Nchini umejikita katika maeneo matano ambayo ni Mazingira ya Biashara, Ubunifu na Teknolijia, Upatikanaji wa Mitaji, Elimu ya Ujasiriamali na Ujuzi na Umuhimu wa Uhamasishaji na Mtandao katika maendeleo ya ujasirimali .

Mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa Linalojihusisha na Maendeleo ya Biashara (UNCTAD), Bw. Lorenzo Tosini alisema shirika hilo limeweka suala la uendelezaji ujasirimali katika ajenda kuu na Tanzania inapofanya hivyo inaendana na ajenda hiyo.

“Katika kukuza ujasiriamali kuna changamoto mbalimbali ambazo nchi nyingi za Afrika zinakabiliana nazo na kuwepo kwa mkakati huo nchini Tanzania itasaidia katika hili,” na kuongeza mkakati huo pia usaidie kuja na sera inayoleta usawa kwa wajasiriamali.

Alisema vikwazo vikuu katika mataifa haya katika ujasiriamali na biashara ni pamoja na vikwazo vya kisheria, upatakanaji wa mitaji kutoka taasisi za kiedha, na uhafifu wa teknolojia na mawasiliano .

## NEEC ni kiongozi katika safari ya kuwawezesha wananchi kiuchumi nchini

Baraza la Taifa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ni chombo cha juu kitaifa chenye jukumu la kuratibu, kufuatilia, kusimamia na kutathimini mikakati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliundwa kwa Sheria ya Bunge namba 16 ya mwaka 2004 kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo Bi, Beng'i Issa anaeleza mambo mbalimbali kuhusu NEEC katika mahojiano aliyofanya na gazeti la mwananchi kama ifuatavyo:

### Ni yapi malengo ya NEEC?

Kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na fursa zinazowazunguka na namna ya kuzitumia, Kuhamasisha wananchi kujingga katika vikundi vya kuweka akiba na kukopa, Kuhamasisha biashara za ubia mionganii mwa Watanzania na wageni pamoja na Kuratibu na kusimamia mfuko wa kumwezesha mwananchi kiuchumi.

Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa uratibu wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa, Wilaya na Sekta binafsi. Mpaka hivi sasa madawati ya uratibu wa uwezeshaji yameanzishwa katika Wizara 20, Idara na Taasisi 58, Mikoa 26 na Halmashauri na Majiji 185, Kuratibu uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mafunzo ya Ujasirimali nchini.

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi ambao mpaka hivi sasa umeweza kudhamini mikopo yenyeye thamani ya Tshs 11billioni. Kuandaliwa kwa utaratibu wa kimfumo wa usimamizi wa VICOBA nchini kwa kushirikiana na TAMISEMI ambapo hivi sasa VICOBA vi-naandikishwa katika ngazi ya Halmashauri zote nchini. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Benki kuu na mashirikisho ya VICOBA nchini linakamilisha utaratibu wa kuvitambua kisheria vikundi hivi vinavyochangia kwa kasi kubwa katika kuondokana na umaskini wa kipato kwa wananchi wa vijiji na mijini.



Kuoanisha Sheria za kisekta ziendane na misingi ya uwezesaji wananchi kiuchumi. Sheria zilizopitiwa hadi sasa ni sheria ya uhamiaji, kazi, uwekezaji, madini, utalii, ujenzi na kilimo.

### **Nini maana ya uwezesaji wananchi kiuchumi?**

Ni uamuzi na hatua mahususi iliyochukuliwa na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuinua uelewa, ujuzi, elimu, hali ya uchumi wa mali na fedha wa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika sera, mipango na mikakati ya kumiliki uchumi wao wenye. Sera ya Uwezesaji inajumuisha wakulima, wavuvi, wafanyakazi na wafanyabiashara katika sekta mbalimbali.

### **Hali ya uwezesaji wananchi kiuchumi ikoje?**

Hali imeboreka sana ukilinganisha na miaka iliyopita kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanya na Serikali katika nyanja za midundombinu ya barabara, umeme, maji, elimu, afya na mawasiliano.

### **Ni ipi nafasi ya NEEC katika kuwawezesha wananchi kiuchumi?**

NEEC ndiyo taasisi kiongozi katika safari ya kuwizesha wananchi kiuchumi nchini kwa kuratibu ushiriki mzuri wa Wizara, Idara, Taasisi, Serikali za Mikoa, Halmashauri na Sekta binafsi nchini. Baraza linaratibu vyema uwezesaji wananchi kiuchumi kupitia mkakati wa kitaifa wa uwezesaji wananchi kiuchumi ambao umeainisha majukumu na matarajio ya wadau wote wa sekta ya umma na binafsi katika kuwzesha Tanzania kiuchumi.

### **Baraza limetekeleza miradi gani yenye lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi?**

Baraza linaratibu miradi mbalimbali inayolenga makundi ya vijana, akina mama, wakulima, wavuvi, wachimbaji wadogo wadogo na wavuvi. Baraza linatekeleza program mbalimbali ikiwamo, uwezesaji kwa vijana inayojlikana kama Young Graduate Entrepreneurship Clinic yenye lengo la kuwzesha vijana wahitimu wa elimu ya juu kupata ujuzi wa kuanzisha na kuendeleza biashara ili kujajiri na kujiri vijana wenzao.

Programu hii hutoa mafunzo, malezi na uungwanishaji na mitaji kwa vijana. Pia, kuna program ya Kijana Jiajiri ambayo inawalenga vijana wenyе umri wa miaka 18-35. Inatekelezwa na Taasisi ya Ushindani na Ujasirimali nchini. Imejikita katika mafunzo (wiki 6), malezi na kuunganishwa na mitaji. Imefanyika kwa majaribio katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Imedhaminiwa na makampuni ya uchimbaji gesi nchini, YBI, Benki ya Barclays na MasterCard Foundation. Vijana zaidi ya 600 wamefikiwa na program hii.

Pia, program ya Ajira Yangu ambayo inalenga Vijana wenyе umri wa miaka 18-35 inatekelezwa kwa ushirikiano wa Baraza na ILO. Hutoa mafunzo ya ujasiriamali na biashara pamoja na malezi kwa miezi 2. Michanganuo ya biashara hushindanishwa na washindi hupatiwa zawadi ya mbegu mtaji. Vijana 50 walishiriki na 20 walishinda zawadi ya Dola 75000. Programu ya Boda Boda kwa Vijana mpango ambao unashawishi vijana kuanzisha SACCOS kujenga tabia ya kuweka akiba na kukopa. Lengo kuwa na SACCOS ya bodaboda kila Mkoa. Kudhamini mikopo ya bodaboda. Inatekelezwa kwa ushirikiano na NSSF. Vijana hupatiwa mafunzo ya ujasiriamali, biashara, usalama na umuhimu wa hifadhi ya jamii. SACCOS 16 zimeanzishwa Dar es Salaam, Kigoma, Rukwa, Mara, Arusha, Mbeya, Dodoma, Ruvuma, Tanga na Geita. Hizi ni baadhi ya program zinazotekelze na baraza kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

**Je, baraza linashirikiana vipi na taasisi zinazotoa mafunzo ya ujasiriamali katika kuhakikisha Watanzania wengi wananaufaika na ujasiriamali?**

Baraza linashirikiana kwa karibu sana na Taasisi za umma na binafsi zinazotoa mafunzo ya ujasiriamali katika kuhakikisha Watanzania wengi wananaufaika na elimu ya ujasirimali. Baraza linashirikiana na Taasisi kama SIDO, VETA, Vyuo vya Elimu ya Juu nchini na Taasisi binafsi za elimu ya ujasirimali katika kuwezesha uratibu mpana wa elimu ya ujasiriamali. Baraza katika kutambua umuhimu wa elimu ya ujasiriamali nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Taasisi ya Elimu Nchini, VETA, Tume ya Vyuo Vikuu, Taasisi ya Usimamizi wa Elimu ya Ufundis Nchini na Taasisi ya Usimamizi wa Mafunzo na kwa Waalimu na ILO kwa pamoja wameandaa Mwongozo wa Ufundishaji Elimu ya Ujasirimali nchini wenyе lengo la kutoa mwongozo unaopimika wa elimu ya ujasiriamali nchini.

## **Kwa kiasi gani sera ya taifa ya uwezesaji wananchi kiuchumi imeleta mabadiliko hasa katika kipindi hiki nchi inaelekea uchumi wa viwanda?**

Sera imeleta mabadiliko chanya hasa katika kuchangia kupungua kwa kiwango cha umaskini katika mahitaji ya kaya hapa nchini kutoka asilimia 34 mwaka 2007 hadi asilimia 28 mwaka 2011. Pia, kiwango cha watu wanaotumia huduma za kibenki kimeongezeza kufikia asilimia 55 ambayo imechangiwa zaidi na matumizi ya huduma za fedha kupitia simu za mikononi. Sera ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi katika kipindi hiki ambacho nchi inaelekea uchumi wa viwanda imekuwa chachu kwa kutoa dira namna ya ushirikishwaji wa Watanzania katika kuwa wamiliki wa sehemu kubwa ya uchumi wao. Ni kupitia sera ya uwezesaji, umuhimu wa Watanzania kushiriki katika fursa za kiuchumi hasa uchumi wa viwanda imetiliwa mkazo na Serikali kupitia mipango ya maendeleo na Dira ya Taifa ya 2025.

## **Ni ipi nafasi ya baraza kuelekea Tanzania ya uchumi wa kati na viwanda?**

Katika kuelekea uchumi wa kati na wa viwanda, Baraza linaratibu ushiriki wa Watanzania katika miradi mbalimbali inayofanyika hapa nchini kwenye sekta zote za kiuchumi kwa kuhakikisha Watanzaniawanashiriki kikamilifu katika kufaidika na fursa hizo. Baraza limechukua jukumu la kuwaunganisha wakulima na wawekezaji kupitia mradi wa ujenzi

wa kiwanda cha sukari mkoani Morogoro unaotekelawa na NSSF na PPF ambapo wakulima wadogo watawezeshwa kuwa wazalishaji wa miwa kupitia kilimo cha mkataba ambacho kinatoa uhakika wa soko ili waweze kuwa washiriki wazuri katika uchumi wa kati na wa viwanda. Pia, Baraza linaratibu program za kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa ndani waweze kufanya biashara katika miradi mikubwa ya uwekezaji hapa nchini, kujengea uwezo Watanzania waweze kuajiriwa katika fani mbalimbali kwenye miradi ya gesi na mafuta na kutoa elimu ya mahusiano bora kati ya wawekezaji na wananchi wanaozunguka miradi ili waweze kufaidika kwa pamoja na uwekezaji husika.

## **Je, NEEC ina mikakati yoyote ya kufanya semina elekezi kwa wananchi na viongozi wa kisasa ili kuelimisha kuhusu dhana yauwezesaji?**

Baraza kupitia Mkakati na Mwongozo wa Kitaifa wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi linaratibu juhudi mbalimbali za Uwezesaji Wananchi Kiuchumi kupitia Mfumo wa Serikali kuanzia Wizara, Idara, Taasisi, Serikali za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Sekta Binafsi nchini.

*inaendelea uk.22*

Mpaka sasa Baraza limeweza kuanzisha madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Wizara zote 19, Taasisi na Idara 58, Mikoa 26 na Halmashauri na Majiji 185 nchini. Tumeweza pia kuendesha mafunzo ya ujengaji uwezo katika madawati hayo katika ngazi zote ili waweze kutekeleza majukumu ya uratibu uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa ufanisi unaotarajiwa katika maeneo yao.

## NEEC yaanika uwezesaji kwa watakao tumia fursa za mradi wa bomba la mafuta.



Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Dkt. John Jingu wa pili kushoto akifasana jambo kuhusu fursa za mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta toka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanga Tanzania, wa pili kulia Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Bi. Beng'i Issa, kushoto Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Huduma za Kifedha na Mikopo-UTT Microfinance PLC, Bw. James Washima na kulia ni Msajili Msaидizi wa Maendeleo na Tafiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Bw. David Jere.

Baraza la Taifa la Uwezesaji wananchi kiuchumi (NEEC) limejipanga kuanza kutekeleza kwa vitendo fursa zitakazotokana na ujenzi wa mradi mkubwa wa Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleni Tanga kwa kuwaelimisha, kuwaonesha na kuwawezesha wananchi watakaotaka kuzitumi fursa hizo.

Baraza la Taifa la Uwezesaji wananchi kiuchumi (NEEC) limejipanga kuanza kutekeleza kwa vitendo fursa zitakazotokana na ujenzi wa mradi mkubwa Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleni Tanga kwa kuwaelimisha,

kuwaonesha na kuwawezesha wananchi watakaotaka kuzitumiafursahizo.

Mradi huo mkubwa uliosainiwa mwezi Mei mwaka huu na kuwekwa jiwe la msingi tarehe 5 Agosti 2017 Chongoleani mkoani Tanga na Rais John Magufuli na Yoweri Museveni wa Uganda unalenga kutoa fursa za kiuchumi kwatanzania.

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi, Dr John Jingu alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwisho mwa juma, kwamba wamejipanga kuwaelimisha, kuwaonesha na kuwawezesha wananchi kuzitumia fursa za ujenzi wa maradi huokuanzisha shughulinnza kiuchumi.

"Tumejipanga vizuri katika kuwaelimisha, kuwaonesha fursa zitakazo kuwepo na kuwapa uwezesha kupitia mifuko ya uwezeshaji 19," serikali imeweka fedha katia mifuko hii hivyo wananchi wanahitajika kuchagamikia, aliongeza kusema Dr Jingu.

Alisema ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kutoa fursa za ajira zaidi ya 10,000 kwa watanzania, na pia amezitaka Taasisi za elimu ya mafunzo ya ufundi stadi ikiwemo VETA kuendelea kuandaa vijana watakao endana na fursa za ujenzi huo.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza hilo Bi. Bengi Issa alizitaja shughuli za kiu-chumi zinazotarajiwa kuwepo katika mradi huo ni biashara za usafirishaji wa bid-haa na watu, ujenzi wa miundombinu mbalimbali, huduma za chakula, uuzaji wa bidhaa za chakula, ulinzi, uuzaji wa vifaa vya ujenzi.

Huduma zingine ni kama vile afya, sheria, fedha, bima, huduma za taka, huduma ukarabati na vifaa vya usalama kazini. Alifafanua kwamba baraza litashirikiana na mikoa ambayo bomba hili linapita kama vile Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga na wilaya 24 na vijiji 184 ili kuhakikisha kwamba wananchi wana shiriki kikamilifu katika mradi huo. "Sisi tumejipanga na tutakuwa karibu na ujenzi huu na fursa zote kadiri zitakavyo zinajitoeza tutazitangaza katika tovuti yetu" na pia watazipata katika halmashauri zao," alisema Bi Bengi Issa.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Huduma za Kifedha na Mikopo-UTT Microfinance PLC, Bw. James Washima alisema kwamba taasisi yake imejipanga kuwawezesha watanzania kupata uwezeshaji wa mitaji kwa wajasiriamali na wafanya biashara ili kuweza kuzitumia fursa katika mradi huo mkubwa. "Tunatoa mikopo ya aina mbalimbali tunawakaribisha kuja kuomba mikopo ili wazitumie fursa za mradi huu wa bomba la mafuta," alisema Bw. Washima. Aliongeza kusema wanaotaka ni vyema kuwa katika vikundi, watapata mikopo wanayotaka ikiwemo ya vitendea kazi na mikopo ya kutekeleza zabuni walizoshida na mafuzo ya ujasiriamali.

Naye Msajili Msaidizi wa Maendeleo na Tafiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Bw. David Jere alisema kwamba wakandarasi wanahitajika kujiunga katika ubia ili kuwa na sifa ya kuingia katika mradi huo mkubwa wa ujenzi wa bomba hilo

## HABARI KATIKA PICHA



Washiriki wakifuatilia majadiliano katika kongamano la ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mh. Sophia Mjema akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa jukwaa la uwezesaji wanawake mkoa wa Dar es salaam.




Waziri wa Nchi,Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wale mavu Mh. Jenista Mhagama akizungumza kwenye Semina ya Wabunge juu ya ushiriki wa Wananchi katika Uwekezaji.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mh.Paul Makonda akizindua programu ya Kijana Jiajiri.

## HABARI KATIKA PICHA



Benki ya Posta Tanzania ikitabidihi zawi ya hundi kama mbegu mtaji kwa washindi wa programu ya Young Graduate Entrepreneurship clinic



Kongamano la pili la Mwaka la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi, Mjini Dodoma



Mafunzo ya Uwezesaji kwa vikundi vya vikoba na SACCOS



Katibu Mtendaji, Bi Beng'I Issa akisaini ma-kubaliano ya ushirikiano na Shirika la hifadhi ya jamii, NSSF yenye lengo la kuwezesha vijana waendesha bodaboda nchini

## HABARI KATIKA PICHA



Mjumbe akizungumza jambo wakati wa majadiliano ya kuunda mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza ujasiriamali nchini.



Mjumbe akichangia mada wakati wa majadiliano ya kuunda mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza ujasiriamali nchini.



Wajumbe wakijadili mapendekezo yao ili kufanikisha mkakati wa kitaifa wa kuendeleza ujasiriamali



Mjumbe akichangia mada wakata wa majadiliano ya kuunda mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza Ujasiriamali nchini.

## **Baraza La Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**S.L.P 1734**

**Mtaa wa kivukoni**

**Dar es Salaam-Tanzania**

**Simu/nukushi:+225 22 2125596**

**Barua Pepe: neec@uwezeshaji.go.tz**

**Tovuti: www.uwezeshaji.go.tz**


**Facebook:NEEC**

**Twiter:neec@empowerment**

**Youtube:Uwezeshaji**



**NEEC**



**NEEC Tanzania**



**Uwezeshaji**